# Utangulizi wa Elimu Mjumuisho kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

Moduli ya

1



## Kitabu cha Washiriki

Umetayarishwa kwa ajili ya:
Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu
The Norwegian Association of Disabled
Umeandaliwa na:
Enabling Education Network, Agosti 2020

NAD – The Norwegian Association of Disabled
MADRASA EARLY CHILDHOOD PROGRAMME
EENET
Inclusive Learning Approach

[Maelezo ya picha: Picha iliyopo katika jalada inaonesha kundi  wamekaa katika viti  katika umbo la mduara, pembeni karibu na ukuta wamekaa viziwi wawili mbee yao yupo mkalimani anawatafsiriwa viziwi hao maneno yanaoyesemwa na mkufunzi. Mkufunzi wa kike amesimama pembeni kulia kwa mshriki ambae ni kiziwi na amevaa kanzu nyeupe. Washiriki wengine wanawake na wanaume wanamsikiliza kwa makini mkufunzi wao.]

Unaruhusiwa kusambaza na kusanifu muongozo huu ili uendane na mazingira uliopo Hata hivyo unapaswa kutoa utambulisho sahihi, chimbuko la idhini, na uoneshe iwapo kuna mabadiliko uliyoyafanya. Unaweza kufanya hivyo kwa namna yoyote inayokubalika, lakini bila kuonesha kuwa mabadiliko au matumizi hayo yamethibitishwa na taasisi inayohodhi haki ya muongozo huu. Huruhusiwi kutumia kitabu hiki kwa lengo la kujinufaisha kibiashara. Iwapo utakihariri kijitabu hiki, kurekebisha, au kuongezea kilichoandikwa humu, utakakipokisambaza unapaswa kutumia idhini halisi kama iliyotumika kabla ya kijitabu kufanyiwa marekebisho Huruhusiwi kutumia kanuni za kisheria au teknolojia ambayo kisheria itawazuia wengine kufanya chochote katika muongozo huu ambacho idhini ya awali imeruhusu. Kwa taarifa zaidi, rejea kwenye kiungo kifuatacho: https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/legalcode

Miongozo hii inapatikana chini ya Leseni ya Creative Commons Non-Commercial

# Yaliyomo

1. Vifupisho....4
2. Je, Kitabu hiki ni kwa ajili ya nini na kwa nani?....5
3. Tunajifunza vipi?....8
4. Ubaguzi....14
5. Je, mfumo wa elimu ni nini?....22
6. Elimu mjumuisho ni nini?....27
7. Vikwazo vya ujumuishaji katika elimu....39
8. Kuwa mtetezi wa elimu mjumuisho....48
9: Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho katika jamii....55
10. Kuendelea kujifunza kuhusu elimu mjumuisho....57

# 1. Vifupisho

| | |
|---|---|
| CBO | Jumuiya za kijamii |
| JWWU | Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu |
| EENET | Mtandao wa kuwezesha elimu |
| NAD | Jumuiya ya watu wenye Ulemavu ya Norway |
| NGO | Jumuiya zisizo za Kiserikali |
| SHIJUWAZA | Shirikisho la Jumuiya za Watu wenye Ulemavu Zanzibar |
| SIT | Timu ya skuli ya ujumuishaji |
| ToT | Mafunzo ya wakufunzi |

## 2. Je, Kitabu hiki ni kwa ajili ya nini na kwa nani?

Kitabu hiki cha muongozo ni kwa ajili ya mafunzo ya msingi katika elimu mjumuisho kwa washiriki kutoka jumuiya za watu wenye ulemavu (JWWU).

Madhumuni ya mafunzo haya ni kuitambulisha elimu mjumuisho kwa wanachama wa jumuiya za watu wenye ulemavu ili wajuwe elimu hiyo ikoje. Yaliyomo katika muongozo huu ni pamoja na mada mbalimbali zilizochukuliwa kutoka kwenye programu tofauti za mafunzo.


Mafunzo haya pia yamelenga kujenga uwezo wa ushawishi na namna bora ambayo washiriki wanaweza kundesha harakati za ushawishi kwa ajili ya elimu mjumuisho katika maeneo yao.

Mafunzo haya ni sehemu ya mchakato wa muda mrefu wa kujenga uwezo kwa jumuiya za watu wenye ulemavu juu ya elimu mjumuisho, na mafunzo ya ziada yataandaliwa kufuatia mafunzo haya.

Elimu mjumuisho **haimaanishi** tu kuwaandikisha watoto wenye ulemavu skuli. Bali ni kuhakikisha kwamba **kila** mwanafunzi **anahudhuria** skuli, **anashiriki** katika harakati za kujifunza na kijamii, na **wanafikia** malengo kulingana na ukomo wa uwezo wao.



[Maelezo ya picha: Mbele wanaonekana watoto wawili, mmoja mwenye ualbino, wamekaa sakafuni wakicheka pakiwa na karatasi kubwa baina yao yenye maandishi na michoro. Nyuma ya picha watoto wawili wa kiume mmoja ana gongo la kutembelea wanabandika bango ukutani. Upande wa kulia watoto watatu wamekaa kila upande wa deski na mwalimu amewaelekea wanafunzi huku akitabasamu. Wote wako darasani ambako kuna karatasi zenye maandishi zilizobandikwa katika kuta].




[Maelezo ya picha: Watoto watatu wakike wanacheza nje na nyuma yao kukiwa na jengo la skuli. Mtoto mmoja amekamata ncha moja ya kamba na mtoto aliye katika kitimwendo akiwa amekamata ncha nyengine ya kamba hiyo. Mtoto wa tatu anaruka kamba hiyo. Wote wanatabasamu ]

# 3. Tunajifunza vipi?

Kabla hatujaanza kutafakari kuhusu elimu mjumuisho, ni muhimu kufikiria jinsi tunavyojifunza – tukiwa watoto au watu wazima. Kufahamu njia tofauti tunazotumia kujifunza itatusaidia kuunga mkono mkabala wa kujifunza kwa ujumuishi, kuanzia mazingira ya nyumbani, katika jamii na skuli pia.

Watu wengi wanadhani kujifunza kunatokea tu pale watoto wanapoanza kwenda skuli, lakini kumbe watoto wachanga na watoto wadogo huanza kujifunza mara tu baada ya kuzaliwa. Fursa nyingi za kujifunza zinapatikana nyumbani na katika jamii na fursa hizi huendelea kuwepo katika kipindi chote cha uhai wetu.

**Kujifunza kunatokea kila mahali, muda wote na kwa kila mtu**

ü Kucheza ni namna bora ya kujifunza kwa watoto wote.

ü Watoto pia hujifunza kwa kusaidia kazi za nyumbani na kushirikishwa katika shughuli za kila siku.

ü Kujifunza hakupo skuli pekee.

ü Huhitaji nyenzo maalumu ili kufanikisha mchakato wa kujifunza nyumbani.

ü Stadi za kijamii, ustawi wa hisia, uratibu wa viungo, na ubunifu vyote hivi hujumuishwa pamoja ili kujenga msingi wa kujifunza (fikiria maneno ya kukumbuka ambayo ni Kijamii, kimwili, kiakili, kibunifu na kihisia)

ü Wazazi na walezi wana ujuzi mwingi ambao wanaweza kuwafunza watoto wao.

Tunajifunza vitu kwa sababu tunataka au tunahitaji kujifunza, tunajifunza kwa kufanya (kutenda), kwa kuiga, na kwa kusaidiwa.

Picha zilizopo katika kurasa zifuatazo zinaonesha kuwa tunajifunza kwa njia tofauti.



[Maelezo ya picha: Watu wawili wamesimama pamoja. Mmoja ana ndevu. Wote wanaosha vyombo na sufuria. Wote wanaimba huku vinywa vyao vikiwa wazi. Kuna dirisha lililo wazi nyuma yao. Ndege anaimba nyuma yao.]

## Tunajifunza nini?

**Stadi za maisha:** Watoto hujifunza stadi muhimu za maisha kwa kufanya kazi za nyumbani. Ni muhimu kwa watoto wa kiume na wa kike kushiriki katika utekelezaji wa majukumu haya ili kuondoa ubaguzi wa kijinsia.

**Msamiati, mashairi na mirindimo:** Kuimba pamoja ni namna nzuri ya kuwafunza watoto  misamiati, mirindimo na mashairi, pamoja na ubunifu.

**Kusikiliza mazingira:** (ndege anaimba dirishani) husaidia watoto kupenda mazingira jambo ambalo ni muhimu katika nyakati hizi ambapo mabadiliko ya tabia nchi yanamuathiri kila mtu.




[Maelezo ya picha: Bibi kizee amekaa katika kitimwendo. Anazungumza kwa ishara kwa kutumia mikono. Viduara vya mazungumzo vinaonesha kwamba anasimulia hadithi au kuelezea ndoto fulani. Katika kiduara cha mazungumzo mtu mmoja anayeonekana kama bibi kizee amelala. Mtu huyo anaota kwamba anaruka angani. Kikundi cha watu wazima na watoto wa umri mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mtoto mmoja mwenye ualblino, wamekaa sakafuni. Nyuso zao zinaonesha kuwa wanamsikiliza bibi kizee kwa makini]

## Tunajifunza nini?

**Msamiati na lugha:** Kusimulia hadithi, ziwe za kubuni au za kweli ni utaratibu mzuri kwa ajili ya kuwasaidia watoto kujifunza lugha, ubunifu na kutafakari kwa kujenga hoja.

**Kuwasikiliza wengine:** Kujifunza kupitia watu wazima na uzoefu walionao huwawezesha watoto kuwapenda na kuwathamini watu waliomo katika familia zao na jamii.

**Utamaduni wa asili**: Kwa kusikiliza hadithi watoto hujifunza kuthamini utamaduni wao wa asili na kujua asili ya tunu (desturi) fulani.



[Maelezo ya picha:  Mtoto anatilia maji mche uliopo kwenye kopo. Kiduara cha maneno chenye alama ya kuuliza kinaashiria mtoto anauliza maswali. Mwanamke ambae ni kijana amesimama kando ya mtoto, akizungumza na kuashiria kwa mikono. Kiduara cha maneno chenye picha ya mmea wenye matunda mengi inaashiria mtoto na mama yake wanajadili kuhusu mmea.]

### Tunajifunza nini?

**Stadi za maisha:** Kujifunza stadi za maisha kama vile jinsi ya kuotesha mimea ni muhimu sana kwa watoto. Watoto pia hujifunza jinsi ya kuvitunza viumbe hai – mmea, na kuuhudumia kila siku.

**Uvumilivu na utafiti:** Mimea humea taratibu, watoto hujifunza uvumilivu na utafiti wakifuatilia ukuaji wake.

**Kujifunza kupitia wengine:** kujifunza kupitia watu wengine katika familia au jamii wenye ujuzi ambao wewe huna.



[Maelezo ya picha: Mtoto mdogo amekaa sakafuni akiwa na gongo la kutembelea kando yake. Amezungukwa na vyombo kadhaa vilivyotengenezwa kwa maada zilizorejeshewa. Kinywa chake kipo wazi na kuna kiduara cha alama ya kuuliza juu ya kichwa chake.]

### Tunajifunza nini?

**Hesabati, sayanzi na fizikia:** Kujifunza kuhusu ujazo, vipimo, kiwango, na pia kuhusu vimiminika na maada.

**Utafiti:** Jinsi gani ujazo na kiwango hubadilika kutoka kwenye chombo kimoja hadi chengine.

**Uratibu wa mwenendo wa viungo na ufahamu:** jinsi ya kumimina kimiminika kwa umakini kutoka katika chombo kimoja hadi chengine.

## Kwa nini ni muhimu kwa falsafa ya elimu mjumuisho kufahamu zaidi namna tunavyojifunza?

Ni muhimu kwa sababu husaidia:

- ü Walimu kutafakari jinsi gani warahisishe mchakato wa kujifunza darasani na skuli
    - Ø Hii hujumuisha kutumia mbinu za **kuchanganyika na ubunifu** darasani, kama vile **kufanya kazi katika vikundi, kutatua changamoto pamoja, na kusimuliana hadithi na kubadilishana mawazo** (mara nyingi huitwa mbinu za ufundishaji zilizoegemea kwa mwanafunzi);
- ü Wazazi na walezi hufikiria ni jinsi gani wanaweza kurahisisha mchakato wa kujifunza nyumbani na katika jamii.
    - Ø Hii inajumuisha kubuni fursa za kujifunza katika mazingira ya nyumbani na jamii kupitia shughuli za kila siku, kama vile **kupika, kuotesha mimea, na kujifunza ujuzi (stadi) mpya kupitia wanafamilia na wanajamii.**




[Maelezo ya picha: Watu watatu wanachezea vitu vilivyotengenezwa kwa maada zilizorejeshewa na tope. Mtoto mmoja wa kike anajenga ukuta kwa kutumia tope na chupa za plastiki. Mtoto mwengine anasukuma gari ndogo iliotengenezwa kwa chupa ya plastiki. Mwanamke ambae bado ni kijana amesimama, akiwa amembeba mtoto. Yupo makini akiwa ameshikilia chupa na kijiti.]

# 4. Ubaguzi

Tunapoelewa zaidi kuhusu mizizi ya ubaguzi, tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuukomesha ubaguzi— kwa mtu yeyote au kikundi chochote.

## Ubaguzi ni nini?

Ubaguzi hutokea wakati makundi ya watu au watu binafsi wanapodhulumiwa au kutengwa katika njia ambazo huwanyima haki sawa na rasilimali.




[Maelezo ya picha: Mwanamke aliyevaa kwa umaridadi akiwa amesimama nje ya jengo la skuli akiashiria muelekeo tofauti na ilipo skuli. Mtoto wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na viatu vya kandambili, akiwa amebeba begi anaangalia chini huku akiondoka katika eneo la skuli. Anaonekana mwenye huzuni. Kwa nyuma kuna mtoto wa kike na wa kiume waliovaa sare za skuli wanazungumza.]

## Ubaguzi unaanzia wapi na kwa nini unatokea?

- **Inawezekana watu wasibaini** kuwa wanabagua; wanaweza kudhani kuwa mitazamo yao na tabia ni za kawaida na zinakubalika.
- Kuna aina nyingi za unyanyapaa katika jamii (mf. Wanawake hawawezi kufanya biashara zao wenyewe); au watoto wenye ulemavu hawawezi kujifunza). Watoto hukuwa wakiwasikia watu wazima wakizungumza kuhusu unyanyapaa kama huu (mf. Watu wenye ulemavu hawawezi kufanya kazi, watoto wa kike hawawezi kufanya vyema katika mtihani wa hesabati, au huwasikia walimu na watu wazima wengine wakiwaita watoto wenye mahitaji maalumu ya elimu na ulemavu 'wazito' au 'wapumbavu'). Watoto huanza kuamini kuwa unyanyapaa huu ndio hali halisi. Wanapokua na wao huiga unyanyapaa huu na kuanza kuutekeleza (mf., kukataa kutibiwa na daktari wa kike kwa sababu wanaamini sio mahiri kama alivyo daktari wa kiume); au hukataa kumfundisha au kumuajiri mtu mwenye ulemavu kwa sababu wanaamini hawafundishiki au hawaajiriki). **Tabia** hii **iliyoegemea katika unyanyapaa ni ubaguzi**.
- Watu wanaweza kubagua **kwa sababu wana hofu**. Kwa mfano, wanaweza kuhofia kwamba kuna makundi ya watu fulani wanaleta mkosi (mf., hofu ya ulemavu kuwa ni laana). Au wanaweza kuhofia kwamba makundi fulani yatahodhi kitu fulani ambacho ni muhimu (mf., watu kutoka bara watapora ardhi ya wazawa). Mara nyingi hofu hii ina misingi ya unyanyapaa na kutoelewa.
- Watu wanaweza kubagua kwa azma ya **kudumisha au kujenga hisia za kujitukuza.** Wanaamini wanaweza kuwa au kusalia wenye nguvu ikiwa watawanyima wengine haki na uhuru.

## Mzunguko wa ubaguzi

**Tukiwa watoto**: Tunapokea kilicho mbele yetu na kile tunachoambiwa (kuhusu jinsia, wakimbizi, watu wenye ulemavu, n.k). Mf. Wanawake hawawezi kufanya kazi za aina fulani, baadhi ya wakimbizi ni 'waporaji wa ardhi', baadhi ya watu wenye ulemavu hawawezi kujifunza.

**Kama kijana :** tunatazama pande zote na kuona 'Ushahidi' kwamba ubaguzi upo kweli, kwa mfano wanawake wachache katika sekta Fulani kama vile uhandisi, watu kutoka bara kuweza kupata ardhi bure,kazi na huduma za kijamii, watu wenye ulemavu kutengwa maskulini.


**Tukiwa watu wazima:** Hujiaminisha kwa kuegemea mitazamo yetu ya kibaguzi, na kuanza kutenda kwa mujibu wa kile tunachokiamini; tunawalea watoto wa kike kwa kuwaandaa kufanya kazi fulani, tunawaangalia wahamiaji kama **wanufaika wasiostahiki**, tunajitenga na watu wenye ulemavu na familia zao. Tunapotenda kwa kufuata Imani zetu, **tunabagua**.

Matendo ya mtu mmoja mmoja huanzisha na kudumisha **mfumo kandamizi** ambao huunda sera, mazingira na taasisi ambazo huyabagua makundi mbalimbali. Watoto huzaliwa na kuyakuta haya na kuanzisha (kuendeleza) upya mzunguko wa ubaguzi.

[Maelezo ya picha:  Katika ukurasa uliopita kuna mchoro wenye visanduku vinne na kila kisanduku kimeunganishwa na chengine kwa mshale.  Ukianzia upande wa kulia wa mchoro kisanduku kilichopo juu kinasema **‘tukiwa watoto** tunapokea kilicho mbele yetu na kile tunachoambiwa (kuhusu jinsia, wakimbizi, au watu kutoka bara, watu wenye ulemavu, n.k). Mf. Wanawake hawawezi kufanya kazi za aina fulani, baadhi ya watu kutoka bara ni ‘waporaji wa ardhi’, baadhi ya watu wenye ulemavu hawawezi kujifunza.  Kisanduku cha upande wa kulia kinasema  **tukiwa vijana** tunaangalia jamii inayotuzunguka na ‘kuthibitisha’ kwamba mitazamo yetu ni sahihi. Mf. Tunaona kuna wanawake wachache katika sekta fulani kama vile uhandisi, **wakimbizi** wanapewa fursa za bure za kupata ardhi na huduma za umma, watu wenye ulemavu wanakataliwa fursa za kujiunga na skuli. Kisanduku cha chini kinasema **tukiwa watu wazima** hujiaminisha kwa kuegemea mitazamo yetu ya kibaguzi, na kuanza kutenda kwa mujibu wa kile tunachokiamini. tunawalea watoto wa kike kwa kuwaandaa kufanya kazi fulani, tunawaangalia watu kutoka bara kama wanufaika wasiostahiki, tunajitenga na watu wenye ulemavu na familia zao. Tunapotekeleza tunachokiamini, tunaishia **kubagua** Kisanduku kilichopo upande wa kushoto kinasema matendo ya mtu mmoja mmoja huanzisha na kudumisha **mfumo kandamizi** ambao huunda sera, mazingira na taasisi ambazo huyabagua makundi mbalimbali. Watoto huzaliwa na kuyakuta haya na kuanzisha (kuendeleza) upya mzunguko wa ubaguzi.]

[Maelezo ya picha: Katika ukurasa ufuatao kuna mchoro wenye picha nne na kila picha imeunganishwa na picha nyengine kwa mshale. Maelezo ‘mzunguko wa ubaguzi’ yameandikwa kati kati ya mchoro. Picha iliopo juu ya mchoro inamuonesha mtoto wa kike aliyevaa mtandio mwekundu kichwani akisafisha sakafu ya chumba huku ndoo ikiwa kando yake. Kuna sofa nyuma yake na picha mbili zilizotundikwa ukutani, moja ikiwaonesha watu wanne (watu wazima wawili na watoto wawili) na nyengine ikiwaonesha watoto wawili. Mtoto wa kiume anapita karibu na mtoto wa kike ambae anasafisha sakafu. Amevaa sare za skuli na amebeba mkoba wa skuli mgongoni. Mtoto wa kike anamuangalia. Anaonekana amehuzunika. Picha ya upande wa kulia inawaonesha watoto wanne wakiwa darasani. Watoto wa kike wamevaa mitandio meupe wamekaa pamoja na wanaangalia picha katika kitabu. Picha iliopo katika kitabu inamuonesha mwanamke akiwa anapika na mwanamme aliyefunga tai huku ameshika begi la ofisini. Muonekano wa sura ya mtoto wa kiume na wa kike unaonesha hali ya kuchanganyikiwa au mshangao. Picha iliopo chini ya mchoro inamuonesha mtoto wa kike aliyebeba mtoto mgongoni na amesimama nje ya jengo. Nyuma ya picha kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli wakiwa karibu na jengo. Picha iliopo upande wa kushoto wa mchoro inamuonesha mwanamke akiwa amevaa shungi jekundu kichwani akiwa amekaa juu ya kiti anakata mboga zilizopo kwenye sufuria. Mtoto mdogo wa kike amekaa kwenye kiti kando yake, nae pia anakata mboga. Sura ya mtoto wa kike inaonesha hana furaha. Sura ya mama yake inaonesha kukata tamaa au mwenye hofu. Wamenyamaza. Karibu yao kuna sufuria.]

# Mzunguko wa ubaguzi



## Haki za binaadamu kama ni msingo wa elimu mjumuisho


Tunapofikiria elimu mjumuisho ni muhimu kukumbuka kwamba kila mmoja ana haki ya kupata elimu.

- Haki za binaadamu ni **dhamana za kisheria** zinazotumika kote ulimwenguni. Zinamlinda mtu mmoja mmoja na vikundi dhidi ya hatua (au wakati mwengine kutokuchukua hatua) ambayo inaingilia uhuru, haki, stahili na utu wao.
- Kila mmoja ni **mwenye haki** –hii ina maana kwamba haki za binaadamu zinamuhusu kila binaadamu. Sote tuna haki sawa.
- Sisi pia ni watoa haki. Hii ina maana kwamba sote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba haki za binaadamu zinaheshimiwa, na hazivunjwi. Serikali zina wajibu mkubwa katika kuheshimu haki za binaadamu, kama ilivyo kwetu sisi kama wazazi na wanajamii. Kwa mfano, ukiwa kama mzazi, mwalimu au mwanajamii tuna wajibu wa kutoa haki ya elimu kwa kila mwanafunzi.'

**Elimu mjumuisho inahusu kuhakikisha kwamba watoto wote waweze kuwepo skuli, kushiriki na kupata mafanikio. Onesha na jadili kuhusu picha.**

**Kwa hivyo, mfumo wa elimu nini?**

# MIFANO YA HAKI ZA BINADAMU




Haki ya uhuru wa kujieleza




Haki ya pumzika na muda wa starehe




Haki ya uhuru wa kutembea




Haki ya ulinzi wa Kisheria



Haki ya elimu




Haki ya kushiriki kisiasa



Haki ya kufanya kazi

[Maelezo ya picha: Picha iliopo katika ukurasa uliopita inaonesha mifano saba tofauti ya haki za binadamu kwa maneno na picha. Kuelekea kulia kuanzia juu mfano wa kwanza ni haki ya kupumzika na kupata muda wa kuburudika. Picha inayofuata ni ya watu watatu wanaocheza mpira akiwemo mwanamke mmoja na mtu mwengine mwenye gongo la kutembelea. Mfano wa pili ni wa 'haki ya ulinzi wa kisheria'. Picha inayofuata inawaonesha watu wanne akiwepo mwanamme mtu mzima, mwanamke, mtoto na mtumiaji wa kitimwendo wakiwa chini ya nembo kubwa ambayo inaonekana kama mtu mrefu mwenye mikono miwili ya hifadhi na neno SHERIA likiwa limeandikwa chini katikati. Mfano wa tatu ni 'haki ya kufanya kazi'. Picha inayofuata ni mchoro wenye vyumba mraba vinne ukiwemo mchoro mmoja wa mtu katika kila chumba mraba. Mtu mmoja anachimba chini kwa pauro, mtu mwengine yupo kwenye kitimwendo na amekaa kwenye dawati, mtu mwengine amevaa kofia na ameshikilia kitu kirefu mkononi, na mtu wa mwisho ni mwanamke ambae amebeba kikapu kichwani ukiwa na mazao ndani yake. Mfano wa nne ni 'haki ya kujumuishwa kisiasa'. Picha inayofuata inaonesha watu sita waliokaa kwenye viti vilivyofuatana katika pande zote mbili za jukwaa zikiashiria mpangilio rasmi wa ukaaji. Neno 'BUNGE' limeandikwa sehemu ya chini kwa herufi kubwa. Katikati kuna mtu mmoja aliyekaa kwenye kitimwendo ambae anatazamana na mtu mwengine aliyesimama. Wote wawili wamechukua vipaza sauti. Mfano wa tano ni 'haki ya elimu'. Picha inayofuata inaonesha vitabu viwili vilivyowekwa kimoja juu ya chengine na kofia ya muhitimu. movement' Mfano unaofuata ni 'haki ya kutembea'. Picha inayofuata inaonesha mchoro wa ramani ya Afrika. Juu yake kuna mchoro wa mtu aliyekaa kwenye kitimwendo nyuma yake kukiwa na alama za matairi ya gari zikiashiria mwendo. Katikati kuna mchoro wa mwanamke akiwa amemshika mkono mtoto, nyuma yao kuna alama za nyayo zikiashiria mwendo, na sehemu ya chini kuna mchoro wa mtu mwengine nyuma yake kukiwa na nyayo zinazoashiria anatembea. Mfano wa saba na wa mwisho ni 'haki ya uhuru wa kuzungumza'. Picha inayofuata inaonesha mchoro wa mtu upande wa kulia akiwa ameshika kipaza sauti na anazungumza kupitia hicho kipaza sauti. Upande wa kushoto kuna watu watatu ambao wamesimama wima, ikiashiria kwamba wanasikiliza.]

## 5. Je, mfumo wa elimu ni nini?

Mfumo wa elimu katika nchi nyingi ni wenye mambo mengi. Unajumuisha vipengele vingi vilivyoungana na vinavyohitaji kufanyakazi pamoja. Mfumo wa elimu pia unahitaji kuungana na sekta nyengine– hauwezi kufanyakazi kwa ufanisi bila ya mashirikiano na sekta nyengine.


Takriban nchi zote zina mfumo wa elimu ambao umekusanya vipengele vingi:

- Sheria na sera zinazohusiana na haki na utoaji wa elimu;
- Mahakama na vyombo vyengine vya kulinda haki hizi
- Idara za serikali, timu au watu binafsi wanaohusika na vipengele mbalimbali vya elimu (mf.bajeti/fedha,mitaala, mitihani, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, maendeleo ya walimu na uajiri, miundombinu);
- Walimu na wahudumu
- Viongozi wa skuli na wilaya, watawala, kamati;
- Vifaa vya elimu (mf.skuli, vituo vya walimu, vyuo, vyuo vikuu);
- Wanafunzi, wazazi,familia na wanajamii;
- Vipengele vyengine kama vile afya, usafiri, teknolojia, n.k

Sehemu zote za mfumo huo zimeungana kwa kiasi fulani. Vitendo au mabadiliko ambayo yanatokea katika sehemu moja ya mfumo wa elimu inaweza kuathiri yanayotokea sehemu nyengine katika mfumo huo. Majaribio ya kufanya mabadiliko katika sehemu moja ya mfumo huenda yasifanikiwe ikiwa hayalingani na mabadiliko katika sehemu nyengine za mfumo huo ( kwa mfano, mabadiliko ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika skuli hayawezi kuwa na ufanisi ikiwa mitaala na mfumo wa mitihani au taratibu za upimaji na tathmini  havibadiliki kulingana na mabadiliko haya mapya katika ujifunzaji na ufundishaji. Kwa hivyo, ili elimu iwe jumuishi Zaidi vipengele vyote katika mfumo wa elimu view na mwekeo mmoja unaofanana.

Pia, mifumo ya elimu haiwezi kufanya kazi bila ya mashirikiano na sehemu nyengine za serikali na jamii. Kwa mfano, kuna haja ya kuwa na mashirikiano na sekta za ustawi wa jamii, afya na sheria; sekta zinazoshughulikia ajira, biashara na uchumi; sekta zenye dhamana ya masuala ya michezo, utamaduni,

mawasiliano na habari; pamoja na sekta zinazoshughulikia uhamiaji na wakimbizi.


Vifaa vya kufundishia na kujifunza
Taarifa za elimu
Maafisa na wasimamizi wa elimu
Wazazi na wanajamii
MFUMO WA ELIMU
Wanafunzi
Walimu na watoa mafunzo
Mitihani na tathmini
SHERIA
SERA
Sheria na Sera
SKULI
Skuli na taasisi za elimu
Bajeti na fedha

[Maelezo ya picha: Picha iliyopo ukurasa uliopita inaonesha mifano kumi tofauti ya mfumo wa elimu kwa maandishi na michoro. Upande wa kulia kutokea juu mfano wa kwanza ni 'takwimu za elimu'. Picha inayofuata ni kioo cha kompyuta na baobonye (keyboard) ambavyo vipo kando ya rundo la karatasi zikiwa na maandishi. Mfano wa pili ni wa 'viongozi waandamizi wa sekta ya elimu na maafisa' Picha inayofuata ni ya rundo la vitabu vikubwa vikiwa mbele ya mtu aliyefunga tai aliyechomoza ambae yupo nyuma ya meza. Mfano wa tatu ni wa 'wanafunzi'. Picha inayofuata ni ya kikundi cha watoto watano na vijana kikijumuisha mwanamke na wanaume, mtu mmoja akiwa kavaa miwani myeusi huku kashika fimbo na mwengine kashika magongo ya kutembelea, na mwanamke ambae kavaa hijabu. Mfano wa nne ni 'mitihani na tathmini'. Picha inayofuata ni ya mchoro wa mtu aliyekaa mezani akiwa kashika kalamu iliyowekwa juu ya karatasi akiangalia chini. Kuna saa nyuma ukutani. Mfano wa tano ni 'bajeti na fedha'. Picha inayofuata ni ya mabunda mawili ya noti ambazo zina alama ya dola za kimarekani juu yake . Mfano wa sita ni 'skuli na taasisi za elimu' na picha inayoambatana nao ni jengo la ghorofa tatu likiwa na madirisha mengi na alama mbele yake inayoashiria kuwa ni 'Chuo Kikuu' na upande wa kulia kuna majengo mawili ya chini yakiwa na mapaa ya bati na milango mitatu iliyofunguliwa katika kila jengo, yakiwa na alama ilioandikwa 'skuli'. Mfano wa saba ni 'sheria na sera'. Picha inayoambatana nayo ni ya marundo mawili ya karatasi. Moja likiwa na maandishi yanayosomeka 'SHERIA' na jengine likiwa na maadishi yanayosomeka 'SERA' . Mfano wa nane ni 'walimu na watendaji wengine wa kada ya elimu'. Picha ilioambatana nao ni ya mchoro wa mwanamke akiwa kashika fimbo ndefu iliyoelekezwa kwenye ubao ulio na maandishi. Mfano wa tisa ni 'wazazi na wanakijiji'. Picha ilioyambatana nao ni ya kikundi cha watu saba akiwemo mwanamke aliyemshika mtoto, mwanamke aliye kwenye kitimwendo, mwanamme mrefu aliyefunga tai na mwanamme mfupi mkakamavu, mwanamke wa tatu na mzee aliyeshika fimbo ya kutembelea . Picha ya kumi ni ya 'vifaa vya kufundishia na kujifunzia'. Picha inayoambatana nayo ni ya vitabu vitatu, kimoja kikiwa kikubwa kuliko vyengine na kitabu chengine kilichobanwa kwa spiringi, rula/mstari, penseli, kalamu na kifutio (raba).

[Maelezo ya picha: Picha inaonesha mchoro wenye maneno 'Sekta ya elimu' katika kisanduku kilicho katikati ya mchoro na mistari inayounganisha kisanduku cha kati na visanduku vyengine vinavyozunguka kisanduku hiki cha kati. Visanduku vinavyoanzia juu kuelekea kulia vinajumuisha mambo yafuatayo; 1. Afya, Marekebisho, 2. Ajira, biashara, maendeleo ya kiuchumi, 3. Ustawi wa jamii, mfumo wa hifadhi/mafao, 4. uhamiaji, wakimbizi, 5. Usafirishaji, 6. Michezo na utamaduni, 7. Idara ya mahakama.]

## Kuungana na sekta nyengine



# 6. Elimu mjumuisho ni nini?

Sote tunaweza kuwa na uzowefu na mawazo mbalimbali kuhusu elimu mjumuisho, lakini katika mtazamo halisi wa elimu mjumuisho, mwanafunzi kamwe sio tatizo; daima mfumo wa elimu ndio tatizo


Mfumo wa elimu ndio tatizo kwa sababu hauna mnyumbuliko na ubunifu unaozingatia mahitaji ya wanafunzi mbalimbali. Mfumo ndio unahitaji kubadilika, sio mwanafunzi.

Picha katika kurasa zifuatazo zinatoa njia mbalimbali za kuangalia kutengwa kwa wanafunzi katika elimu.


Mchoro wa kwanza unaonesha jinsi mfumo wa elimu ya jadi unavyowazingatia wanafunzi walio tofauti kwa kiasi fulani. Viduara vya mazungumzo vinanonesha namna ambavyo walimu katika skuli ambazo **si** jumuishi zinavyoweza kuwapa majina wanafunzi ambao hawawezi kujifunza vizuri au hawapati mafaninkio, kwa mfano mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ya kielimu au ulemavu. Katika mtazamo wa kijadi mwanafunzi anaonekana kuwa ni tatizo. Hii hupelekea skuli na walimu kujaribu kufikiria masuluhisho kwa kuleta mabadiliko kwa mwanafunzi, kujaribu 'kumtibu', au kwa kumfanya kwa namna fulani aweze kuendana na mfumo uliopo.

Mchoro wa pili unaonesha mtazamo mbadala. Hapa mwanafunzi sio tatizo. Mfumo wa elimu ndio tatizo kwa sababu hauko rafiki na hauna ubunifu wa kutosha kukidhi matakwa ya wanafunzi mbalimbali. **Mfumo ndio unahitaji marekebisho na sio mwanafunzi.**

## Mwanafunzi kama tatizo




[Maelezo ya picha: Mtoto wa kike amekaa sakafuni huku kichwa chake akiwa amekifunika kwa mikono yake kwa hivyo huwezi kuuona uso wake. Kuna mikono minne kutoka pembe nne za picha ambayo yote inamnyooshea yeye kidole. Kuna viduara vinne vya maelezo vilivyoambatana na mikono. Maneno yaliomo kwenye viduara yanasomeka “anahitaji vifaa maalumu”, “hasomesheki”, “mzito sana”, na “hawezi kujifunza”]






[ Maelezo ya picha: Picha katika ukurasa uliopita inaonesha mchoro wenye maneno 'Mfumo wa elimu kama tatizo' yakiwa katika kisanduku kilichopo katikati na mistari inayounganisha kisanduku cha kati na visanduku saba vinavyozunguka kisanduku hicho. Visanduku kuelekea kulia kuanzia juu vinajumuisha yafuatayo; 1. Mitazamo ya walimu huzuia mwanafunzi kufanikiwa, 2. Mbinu za kufundishia zisizobadilika, mtaala usiobadilika ambao haukidhi mahitaji ya wanafunzi wote, 3. Mazingira yasiofikika, 4. Watoro wengi, wanafunzi wengi wanaorudia darasa, inaonesha kwamba mfumo wa elimu unahitaji kuboreshwa, 5. Walimu na skuli hazisaidiwi na serikali kwa hivyo haziwezi kukidhi mahitaji ya wanafunzi, 6. Wazazi/wasimamizi/walezi hawashirikishwi, 7. Ukosefu wa visaidizi vya kufundishia na vifaa, 8. Mafunzo hafifu ya walimu yanasababisha mahitaji ya wanafunzi yasitimizwe.]

[Maelezo ya picha: Picha ya ukurasa unaofuata inaonesha mifano minane tofauti ya mfumo wa elimu kama tatizo. Baadhi ya mifano inalingana na michoro iliopita na myengine ni tofauti. Kuelekea kulia kutoka juu:


- mfano wa kwanza unamuonesha Mtoto wa kiume aliyevaa sare za skuli, huku amebeba begi akipanda ngazi. Kwenye ngazi limeandikwa neno 'SEKONDARI'. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Akiwemo mtoto mmoja wa kiume ambae anamuangalia mtoto mwengine wa kiume akielekea juu, mtoto mwengine wa kiume akiwa amevaa miwani myeusi, ameshika fimbo akielekea upande mwengine na mtoto wa kike akiwa amebeba mtoto mgongoni huku akiwa na huzuni na akiangalia upande mwengine. Chini ya ngazi limeandikwa neno 'MSINGI'.
- Mfano wa pili unawaonesha watoto 10 wa kike na 10 wa kiume akiwepo mmoja anaetumia gongo la kutembelea na mwengine mwenye ulemavu wa ngozi, wakiwa wamesimama kwenye foleni wakisubiri zamu yao kutumia maliwato (choo). vyoo vyenyewe vimechakaa. Upande wa kushoto kuna mtoto akijisaidia haja ndogo kichakani. Jengo la skuli lipo kwa nyuma.
- Mfano wa tatu unamonesha mtoto wa kiume amekaa kwenye kitimwendo, akiangalia chini. Kuna ngazi ndefu ya kupanda ili kufika darasani. Kupitia mlangoni anaonekana mwalimu akiwa darasani anaendelea kusomesha.
- Mfano wa nne unaomuonesha mwanamke amesimama mbele ya wanafunzi ambao wamekaa katika madawati yao. Anaonesha juu, anazungumza huku akiwa amewaelekezea mgongo wanafunzi. Katika mstari wa mbele darasani kuna mwanafunzi mmoja anaangalia nje kupitia dirishani na mwengine amejiinamia.
- Mfano wa tano unaonesha rundo la vitabu vitatu, rula, penseli, peni na kifutio, vyote vikiwa vimezungushiwa duara na mstari uliokatisha kati kati ya duara.
- Mfano wa sita mtoto wa kike aliyebeba mtoto mgongoni na amesimama nje ya jengo. Nyuma ya picha kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli wakiwa karibu na jengo. Nyuma kabisa kuna mwalima alivaa shungi jekundu anaonekana akiingia darasani katika jengo lilipo kushoto. Pia kuna mtoto wa kiume alivaa sare za skuli pamoja na mkoba mgongoni anaonekana akielekea katika jengo lilipo upande wa kulia. Kuna mwanamume anaonekana anatembea katika uwanja wa kuchezea.
- Mfano wa saba unaonesha darasa lililojaa wanafunzi kupita kiasi. Mwalimu anaonekana kwa mbali akiashiria katika maandishi ubaoni. Kuta za darasa na madirisha ni chakavu.
- Mfano wa nane unaonesha picha mbili zikiwa zimepambanuliwa (zimetenganishwa) na mstari. Picha ya kushoto inaonesha jengo lenye


maneno yanayosomeka SERA ZA ELIMU. Jengo lipo nyuma ya uzio wa waya. Kupitia dirishani kunaonekana marundo ya karatasi zilizotawanyika. Picha ya upande wa kulia inamuonesha mwanamke na mwanamme wakiwa nje ya nyumba iliyoezekwa kwa nyasi. Mikono yao ipo hewani ikiashiria kutofahamu jambo fulani. Juu ya mkeka kuna mtoto aliyelala ambae ana mguu mmoja.]














# MFUMO WA ELIMU NDIO TATIZO












## Kuna tofauti gani baina ya elimu maalum, ubaguzi, mchanganyiko na elimu mjumuisho?


Elimu mjumuisho mara nyingi hudhaniwa kuwa na maana sawa na elimu mchanganyiko lakini hazifanani. Elimu mjumuisho inashughulikia zaidi ya kuwapigania watoto waliotengwa kufika skuli. Ni lazima pia waweze kushiriki na kupata mafanikio. Ili kila mtoto aweze kushiriki na kupata mafanikio, tunahitaji elimu bora, njia za kufundishia na kujifunzia zinazomzingatia mwanafunzi.

### Elimu maalum au kutenganisha

Kuna mfumo wa elimu kwa wanafunzi 'wa kawaida' (vipande vya duara); na mfumo tofauti kwa wanafunzi wenye 'mahitaji maalum'(vipande vya mraba).



Skuli ya 'kawaida'




Skuli maalum

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo mviringo  na vipande vidogo vidogo vya mviringo vikipita katika vishimo hivyo. Hii inawakilisha skuli ya kawaida. Kipande chengine cha ubao kina vishimo vya mraba na vipande vidogo vidogo vya mraba vikipita katika vishimo hivyo. Hii inawakilisha skuli maalum. Vipande vidogo vidogo vya mraba na mviringo vinawakilisha wanafunzi]

### Mchanganyiko

Hapa watu wanajaribu kubadilisha wanafunzi ili waendane na mfumo unaoitwa wa 'kawaida'(kuvirekebisha vipande vidogo vya mraba viweze kupita katika vishimo vya mviringo). Mfumo wa elimu na utaratibu wa ufundishaji na ujifunzaji haubadiliki. Kwa hivyo, mwanafunzi ni lazima abadilike au ashindwe kufaulu.




Integrated school Skuli mchanganyiko

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo mviringo na vipande vidogo vidogo vya mviringo vikipita katika vishimo hivyo. Kipande kimoja kinakosekana. Pembeni yake kuna kipande kidogo cha mraba ambacho kinawakilisha mwanafunzi wa skuli maalum. Kipande hiki kinarekebishwa ili kiwe na umbo la mviringo na kiweze kuingia katika vishimo vya mviringo. Mchoro huu unawakilisha skuli mchanganyiko ]

## Elimu mjumuisho

Hapa, wanafunzi wote ni tofauti na wote wanaweza kusoma hapa kwa kadiri ya uwezo wao. Mfumo wa elimu umebadilishwa kuweza kushughulikia wanafunzi wote. Mfumo huu unatatua vikwazo vyake vya kujifunza na kushiriki, ikiwa ni kwa sababu ya mitazamo, mazingira duni, mazoea na sera zisizofaa, au ukosefu wa nyenzo.



Skuli jumuishi

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo vya maumbo mbalimbali na vipande vidogo vidogo mbalimbali vikipita ndani ya vishimo hivyo.]

## Visa mafunzo vya ‘Je, hii ni elimu mjumuisho?’

Soma kila moja kati ya hadithi zifuatazo na amua ikiwa unafikiri ni mfano wa elimu mjumuisho, elimu mchanganyiko, elimu maalum iliyotenganisha au iliyowatenga wanafunzi.

**Hadithi ya 1:** Baadhi ya watoto wa kike wenye ulemavu na wasio na ulemavu waliacha kwenda skuli kwa sababu walikua wanaugua mara kwa mara. Baada ya uchunguzi ilibainika kwamba, wanapokua skuli walikua hawatumii vyoo vya mashimo na jambo hili lilidhoofisha afya zao. Vyoo vilikuwa mbali, na havina milango au maji tatizo lililowafanya watoto wa kike waogope kuchokozwa au kubakwa wakiwa chooni, na wanafunzi wa kiume wa eneo hilo. Vyoo pia vilikuwa havifikiki kwa baadhi ya watoto wa kike wenye ulemavu. Wanafunzi wa kike walipopeleka malalmiko yao kwa mwalimu mkuu, mwalimu mkuu alizungumza na asasi isiyo ya kiserikali ambayo ilikua inasaidia miradi ya elimu katika eneo hilo, na wakakubaliana kuweka milango imara yenye kufuli vyooni, na chengine kirekebishwe na kuwekewa reli za kujishikia ili kifikike kwa urahisi na watu wenye ulemavu. Mwalimu mkuu akaanza kuvifunga vyoo ili wanafunzi wa kiume wasiingie; watoto wa kike pekee wangepewa funguo. Mwalimu mkuu ndiye aliyekua akikaa na funguo, kwa hivyo watoto wa kike walikwenda kuchukua funguo kutoka kwake kila wanapohitaji kutumia vyoo.

**Simulizi 1: Hii ni kutenga** –ijapokua sio wa kwa kukusudia. Mwalimu mkuu alikua anajaribu kutatua tatizo ambalo likisababisha watoto wa kike wasiende skuli, lakini kwa bahati mbaya suluhisho likawa pia la kibaguzi.

**2 Hadithi ya 2:** Mwalimu ana watoto 50 katika darasa lake. Mbinu kuu ya kufundishia anayoijua ni kusimama mbele ya darasa na kuwahutubia watoto. Akabaini kwamba watoto wengi hawafahamu anachokisomesha. Licha ya changamoto ya kuwa na samani duni darasani, amejaribu kubadili mpangilio wa wanafunzi darasani mara kadhaa, na sasa ameamua kuwaweka mbele wale wanaofahamu haraka na ndiwo ambao huwauliza maswali mara kwa mara kwa sababu wanafunzi wengine wanaonekana hawajishughulishi.

**Hadithi ya 2: Hii ni elimu mchanganyiko**–Mwalimu anaruhusu wanafunzi wenye ufahamu hafifu kubaki darasani, lakini yeye mwenyewe habadili mbinu zake za ufundishaji, kwa hivyo wanafunzi hawa wanahudhuria bila kushiriki au kujifunza chochote. Alijaribu kufanya marekebisho ili darasa liwe jumuishi (mf. Kubadili mpangilio wa ukaaji) lakini akakata tamaa baada ya kubaini

hakujabadili matokeo, badala ya kufikiria njia mbadala za kutatua changamoto inayomkabili.

**Hadithi ya 3:** Mwalimu alikuwa na changamoto ya kudhibiti kikundi cha wanafunzi wa kiume darasani. Wanaonekana walipoteza hamu ya kujifunza, hawawezi kutulia na mara nyingi humkatisha mwalimu na wanafunzi wengine. Mwalimu aliwatoa darasani nyumbani na kuwaagiza wakae nje ya darasa lakini wakaanza kuzurura mitaani na kuingia matatizoni zaidi. Hawakuwapeleka wazazi wao. Baada ya kutokea hivi mara mbili, mwalimu alikasirika na watoto walikua hawajifunzi ipasavyo. Mwalimu mkuu aliamua kuanzisha darasa jipya kwa ajili ya 'watoto watukutu' kama hawa, hata hivyo ilikua vigumu kumshawishi mwalimu yeyote kwenda kufundisha katika darasa hili, hii ilipelekea watoto waache kabisa kwenda skuli.


**Simulizi 3: Hii ni kuwatenga na kuwatenganisha –**Watoto walitolewa katika darasa la kawaida. Suluhisho lilionekana ni kuwafundisha peke yao, hata hivyo mbinu hii haikufanikiwa na watoto waliamua kuacha skuli, kwa hivyo wametengwa.

**Simulizi 4:** Yusuf ana changamoto ya kujifunza; anapata shida kujifunza hesabati na kusoma. Yusuf anahitaji apate usaidizi wa mtu maalumu ambae atamfafanulia, kinachofundishwa darasani. Hii ni changamoto kubwa kwa mwalimu kwa kuwa darasa lina wanafunzi 40 na lipo mbali kijijini likiwa na nyenzo chache pia. Hata hivyo, mwalimu amemuambatanisha na mwanafunzi mwenzake ambae anafurahia 'kuigiza kama mwalimu' nae anaelewana nae. Mwalimu pia amemruhusu Yusuf kufanya majaribio yake ya darasani kwa kutoa majibu bila ya kuandika. Mwalimu pia amemtafuta mtu mzima hapo kijijini ambae alikua mhasibu. Mtu huyu huja darasani na kufundisha kwa kujitolea kwa saa moja kwa wiki wakati wa vipindi vya hesabati, akimsaidia Yusuf na wanafunzi wengine wenye mahitaji maalumu.

**Simulizi 4: Hii ni elimu mjumuisho** – mwalimu anatumia usaidizi rika kama mbinu ya kumsaidia Yusuf, amebuni mfumo rafiki wa kumtathmini kila mwanafunzi, na kumpatia Yusuf na wanafunzi wengine msaada wanapouhitaji.


**Simulizi 5:** Halima ana umri wa miaka 7 na ana Sura mfanano. Anaweza kuzungumza maneno machache lakini mara nyingi hutumia ishara kuwasiliana – amejifunza pia lugha ya alama kidogo kutoka kwa mjomba wake ambae ni kiziwi. Watoto wengine wanapenda kucheza nae kwa sababu ni mcheshi. Kwa kuwa anaweza kujieleza kwa kuigiza, wanamfahamu akizungumza. Hata hivyo mwalimu wake anahisi Halima ni mchekeshaji na anaonelea ni bora awaamuru wazazi wake wabaki nae nyumbani ili asiwasumbue watoto wengine. Kwa kuwa Halima hawezi kuzungumza vizuri, mwalimu wake hamuulizi swali lolote na humuacha afanye chochote anachojisikia.

**Simulizi 5: Hii ni elimu mchanganyiko** – Halima anaruhusiwa akae darasani lakini mwalimu habadilishi mazingira ili kumsaidia kushiriki na kujifunza.




[Maelezo ya picha: Kuna wanyama watano waliojipanga mbele ya mti mkubwa. Wanyama wenyewe kutoka kushoto ni ndege, kima, ngwini ( penguin), tembo (ndovu), samaki ndani ya bakuli lenye maji, *seal* na mbwa. Kuna mtu aliyekaa kwenye dawati akiwa amewaelekea wanyama. Anawaambia kwamba ‘ili kutenda uadilifu katika tathmini kila mnyama atapaswa kufanya mtihani: tafadhali pandeni juu ya mti’]

**Usawa – kumchukulia kila mmoja kuwa ni sawa na mwengine bila kujali mahitaji maalumu aliyonayo si mara zote kwamba kunaleta ujumuishwaji.**




[Maelezo ya picha: Picha imejigawa sehemu mbili. Picha iliyopo upande wa kushoto inawaonesha watu watatu wakiangalia mpira wa miguu wakiwa nyuma ya uzio. Mtu mmoja mrefu amesimama juu ya sanduku na ameupita ukuta kwa kimo, mtu mwengine mfupi amesimama juu ya sanduku akichuchumia kwa vidole vyake na kichwa chake kimepitiliza kimo cha uzio. Mtu wa tatu yupo kwenye kiti mwendo na uzio umemzuia kabisa kuona mbele. Picha ya upande wa kulia inawaonesha watu hao hao watatu. Safari hii yule mtu mrefu hajasimama juu ya kitu chochote na bado kichwa chake kimepitiliza kimo cha uzio. Yule mtu mfupi amesimama juu ya masanduku mawili na anaweza kuona vizuri zaidi ndani ya uzio. Kuna ngazi/baraza mtelezo (rampu) kubwa kwa ajili ya kitimwendo na kitimwendo kipo juu ya ngazi mtelezo kwa hivyo mtumiaji wa kitimwendo anaweza kuona vyema ndani ya uzio.]

**Elimu mjumuisho inahitaji utekelezaji wa dhana ya ‘usawiya/uwiano’ – kuwawezesha watu kwa namna tofauti kwa mujibu wa mahitaji yao**

# 7. Vikwazo vya ujumuishaji katika elimu

Tunapofikiria kuhusu vikwazo vya ujumuishaji, mara nyingi huwa tunafikiria kuhusu vikwazo vya kimazingira kama vile ngazi na kukosekana kwa baraza mtelezo (rampu). Hata hivyo, vikwazo vikubwa vya ujumuishaji katika elimu inawezekana sio vya kimazingira tu–vinaweza kusababishwa na mitazamo hasi, au kutokana na sera za serikali au skuli ambazo zina ubaguzi, au kwa mazoea ya ufundishaji ambayo hayawezeshi wanafunzi wote kuweza kushiriki, au kutokana na ukosefu wa rasilimali watu na vifaa. Baadhi ya vikwazo vinahitaji pesa ili tuweze kuviondoa (kama vile kujenga baraza mtelezo au kuchapisha vitabu vinavyoweza kufikika). Hata hivyo, vikwazo vingi vinaweza kuondolewa bila ya kutumia pesa nyingi, lakini badala yake tunaweza kutumia fedha chache zilizopo kwa uangalifu katika kutafuta suluhisho lisilo na gharama kubwa.

## Aina za vikwazo vya ujumuishaji

**Vikwazo vya kimazingira:** Hivi ni pamoja na majengo ya skuli, mazingira ya nje na vyoo ambayo hazifikiki au haziko salama, mazingira chini ya kiwango au ya hatari.




[Maelezo ya picha: Mtoto wa kiume amekaa kwenye kiti mwendo, akiangalia chini. Kuna ngazi ndefu ya kupanda ili kufika darasani. Mwalimu anaonekana akiwa darasani anaendelea kusomesha.]

**Kikwazo cha mtazamo:** mf. hofu, fedheha, aibu, au matarajio yaliofifia kwa familia, mitazamo hasi ya watendaji wa skuli na wazazi, mitazamo hasi ya wanajamii.



[Maelezo ya picha: Mtu mzima mwanamme amekaa mbele ya zunna lililowekwa kwenye meza ndogo. Mtoto wa kiume akiwa amevaa sare za skuli amechukua karatasi mkononi akijaribu kumkabidhi mtu mzima. Mtu aliyekaa anaonekana kuzipuuza na kurusha mikono hewani. Sura yake inaonesha ameghadhibika.]

**Vikwazo vya kisera:** mf. Ratiba za skuli zisizo nyumbulifu; ukosefu wa mafunzo ya ziada ya lugha, sheria za elimu zilizopitwa na wakati na sera.





[Maelezo ya picha: mbele ya picha mtoto wa kike aliyebeba mtoto mgongoni na amesimama nje ya jengo. Nyuma ya picha kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli wakiwa karibu na jengo. Nyuma kabisa kuna mwalima alivaa shungi jekundu anaonekana akiingia darasani katika jengo lilipo kushoto. Pia kuna mtoto wa kiume alivaa sare za skuli pamoja na mkoba mgongoni anaonekana akielekea katika jengo lilipo upande wa kulia. Kuna mwanamume anaonekana anatembea katika uwanja wa kuchezea.]

**Vikwazo vya kiutendaji:** mf. Kutotumia mbinu husishi, kutotumia mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunzia, kutofahamu njia tofauti za kujifunza.




[Picha ya 4: Mwanamke amesimama mbele ya wanafunzi ambao wamekaa katika madawati. Anaonesha juu, anazungumza huku akiwa amewaelekezea mgongo wanafunzi. Katika mstari wa mbele darasani kuna mwanafunzi mmoja anaangalia nje kupitia dirishani na mwengine amejiinamia kwenye dawati.]

**Vikwazo vya taarifa** mf. Wazazi na walezi hawafahamu kuwa mtoto wao anaweza kuandikishwa katika skuli iliopo mtaani kwao; elimu mjumuisho haitolewi (haitekelezwi) maskulini; skuli haziwasiliani mara kwa mara na wazazi.





[Maelezo ya picha:  Picha mbili zikiwa zimepambanuliwa (kutenganishwa) na mstari. Picha ya kushoto inaonesha jengo lenye maneno yanayosomeka SERA ZA ELIMU. Jengo lipo nyuma ya uzio wa waya. Kupitia dirishani yanaonekana marundo ya karatasi zilizotawanyika. Picha ya upande wa kulia inamuonesha mwanamke na mwanamme wakiwa nje ya nyumba ilioezekwa kwa nyasi. Mikono yao ipo hewani ikiashiria kutofahamu jambo fulani. Juu ya mkeka kuna mtoto aliyelala ambae ana mguu mmoja.]

**Kikwazo cha nyenzo:** mf. Uhaba wa walimu, wingi wa wanafunzi darasani, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ukosefu wa maliwato yalio safi, salama na yenye kufikika.



[Maelezo ya picha: Darasa lililojaa wanafunzi kupita kiasi. Mwalimu anaonekana kwa mbali akiashiria kitu ubaoni. Kuta za darasa na madirisha ni chakavu.]




[Maelezo ya picha: kuna vyoo viwili, kimoja cha wanawake na chengine cha wanaume.Watoto 10 wa kike na 10 wa kiume akiwepo mmoja anaetumia gongo la kutembelea na mwengine mwenye ulemavu wa ngozi, wakiwa wamesimama kwenye foleni wakisubiri zamu yao kutumia maliwato (choo). vyoo vyenyewe vimechakaa. Upande wa kushoto kuna mtoto akijisaidia haja ndogo kichakani. Jengo la skuli lipo kwa nyuma.]

## Kuhudhuria, kushiriki na mafanikio

- Elimu mjumuisho **haimaanishi** tu kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wapo skuli.
- Bali ni kuhakikisha kwamba wanafunzi **wote** wenye ulemavu (wa kike na kiume, wanafunzi kutoka kwenye makundi ya walio wengi na wachache, wanafunzi walio wakimbizi na wanaoomba hifadhi, waliokimbia makaazi yao, wanafunzi wenye matatizo ya kiafya, wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu, wanafunzi walio mtaani na wanaofanya kazi, mayatima....n.k) ***wanahudhuria*** katika taasisi za elimu (maandalizi, msingi, sekondari, n.k) ***wanashiriki*** katika shughuli za kitaaluma na kijamii, na ***wanafanikiwa*** kufikia ukomo wa uwezo wao wa kujifunza.



[Maelezo ya picha: Mbele wanaonekana watoto wawili, mmoja mwenye ualbino, wamekaa sakafunu wakicheka pakiwa na karatasi kubwa baina yao yenye maandisho na michoro. Nyuma ya picha mtoto mmoja wa kike na mwengine wa kiume mwenye magongo wakiwa wanabandika bango ukutani. Upande wa kulia watoto watatu wamekaa kila upande wa deskin a mwalimu akitabasamu na kuwaelekea wanafunzi. Wote wako darasani ambako kuna karatasi zenye maandishi zilizobandikwa katika kuta ].

Hivyo, tunapojaribu kuelewa vikwazo vya elimu mjumuisho, tunahitaji kuchambua:

- vikwazo vinavyowazuia mahudhurio ya wanafunzi (kufika) skuli
- vikwazo vinavyowazuia **kushiriki** katika kujifunza darasani;
- vikwazo ambavyo vinawazuia kufikia mafanikio kwa mujibu wa uwezo wao ( tukumbuke kuwa mafanikio  hayapimwi kwa alama za mitihani tu, bali pia yanapimwa kwa stadi za kijamii, michezo n.k.)

Katika kurasa zifuatazo kuna picha tofauti ambazo wanafunzi walipiga kuonesha mifano ya elimu mjumuisho au vikwazo vinavyoathiri elimu mjumuisho.

Kila mtu ana tafsiri tofauti ya hali ilivyo. Wanafunzi, walimu, wazazi, walezi, n.k., wanaweza kuwa na tafsiri tofauti kwa hali moja, jambo linalopelekea kuwa na mawazo tofauti kuhusu vikwazo ni vipi na lipi liwe suluhisho.

Taarifa zilizopo chini ya picha zinaelezea kinachooneshwa, kwa mujibu wa maelezo ya waliopiga picha hizo.



- Hii ni barabara hatari ambayo wanafunzi wanapaswa kukatisha ili wafike skuli.
- Madereva huendesha kwa kasi sana. Madereva wanapaswa kuelekezwa kupunguza mwendo wanapokaribia eneo la skuli.

[Maelezo ya picha: Watoto watatu wa kike wakiwa wameshikana mikono. Wanakatisha barabara. Gari linakaribia na lipo karibu sana na watoto.]



- Maeneo ya skuli kama ulivyo uchochoro/ koridoo hii ni kikwazo kwa ujumuishi, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuwatishia wengine ambao ni wadogo na/au dhaifu.

[Maelezo ya picha: Watoto wawili wa kiume wamesimama kwenye koridoo nyembamba yenye giza.]



- Maji safi, salama na yanayofikiwa yanahitajika. Bila ya maji wanafunzi wanasema hawawezi kumaliza vyema siku, hawawezi kutafakari, hawawezi kunawa mikono baada ya kujisaidia, jambo ambalo hupelekea wapate maradhi, magonjwa, n.k.
- Ardhi inayozunguka mfereji sio tambarare, kwa hivyo maji hayafikiwi na wote, mf. Hayawezi kufikiwa na wanafunzi wasioona na wale wanaotumia vitimwendo.

[Maelezo ya picha: Ndoo mbili za chuma zikiwa zimejazwa maji zipo chini ya mfereji. Ardhi inayozunguka mfereji ni ya udongo ikiwa na mawe makubwa.]




- Kuna maliwato mengine kwa ajili ya watoto wa kike ambayo hayaonekani katika picha.
- Wanafunzi waliopiga picha hizi wamefurahi kwa sababu sasa wana maliwato – kabla ilikua ni ardhi tupu bila mahali pa kujisaidia.

[Maelezo ya picha: Kuna eneo kubwa la wazi lililo tambarare. Ni ardhi tupu isiyo na mimea. Majengo matatu tofauti ya choo yamejengwa upande mmoja wa eneo hilo. Kila jengo lina matundu mawili ya kujisaidia.]



- Vitabu visivyofikika: Wanafunzi hawawezi kuvifikia kwa urahisi kwa sababu ya mahali na jinsi vilivyowekwa. Hakuna maandishi ya nukta nundu, ni vitabu vyenye maandishi ya kawaida (vilivyochapwa) pekee.
- Kuwa na vitabu vya kutosha ni jambo zuri kwa sababu wanafunzi hawatohitaji kushirikiana kwa kitabu kimoja.

[Maelezo ya picha: Kuna makabati matatu ya vitabu. Marundo ya vitabu/vijitabu vimekaliana kwenda juu. Makabati yamejaa. Hauonekani mgongo/jina la kitabu.]

# 8. Kuwa mtetezi wa elimu mjumuisho

## Utetezi ni nini?




***Inaaminika haiwezekani, mpaka unapothubutu kufanya***
**Nelson Mandela**

[Maelezo ya picha: Kuna picha ya Nelson Mandela. Chini ya picha kuna nukuu ambayo aliisema. Nukuu inasema “Inaaminika haiwezekani, mpaka unapothubutu kufanya”]

Utetezi unahusu **kuchukua hatua za kuleta mabadiliko** na sisi sote tunakuwa ni watetezi wakati tunapofanya jambo la kuleta mabadiliko, hata kama ni dogo.
Mara nyingi utetezi huhusisha **kuwasaidia watu kupaza sauti zao** katika kuleta mabadiliko katika namna ambavyo watu hufikiri (mitazamo) na namna ambavyo mambo yanafanywa(mazowea).

## Zifuatazo ni baadhi ya nukta nyengine muhimu kuhusu utetezi

- Utetezi ni kushawishi muelekeo wa maamuzi yanayofanywa (mf., sera ya skuli).
- Utetezi ni kusaidia kubadili utaratibu wa jinsi mambo yanavyofanywa (matendo/utekelezaji) ikiwemo jinsi taasisi (mf., skuli) inavyofanya kazi.
- Utetezi unahusisha michakato rasmi (mf., kuchangia katika uundaji wa sera mpya ya serikali) au michakato isiyo rasmi (mf., kuzungumza msikitini kuhusu haki za watu wenye ulemavu).




[Maelezo ya picha: Kikundi cha watu kimekaa katika mpangilio maalumu wakimuelekea mzungumzaji (Spika) ambae hayupo kwenye picha. Kikundi kinajumuisha mwanamke mmoja aliyekaa kwenye kitimwendo ambae anaandika, mtu mwengine mwenye ulemavu wa ngozi ambae amenyoosha mkono na mwanamke mwenye hijabu ambae nae amenyoosha mkono. Watu wengine wawili wameelekeana na wanazungumza jambo. Chini ya picha kuna neno BUNGE likiwa limeandikwa kwa herufi kubwa.]

- Watetezi ni watu ambao huchukua hatua ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.
- Watetezi wanaweza kufanya kazi kwa lengo la kubadilisha maisha yao, familia zao, jamii, nchi, au dunia nzima.
- Watetezi hujenga uhusiano na kuwatambua washirika ili wajenge ushirikiano na mitandao ndani ya jamii yao na kwenye jamii nyengine.




[Maelezo ya picha: Watu watatu wamesimama wanazungumza. Mwanamke ambae yupo upande wa kulia anatumia mikono yake kutoa ishara kwa mwanamme aliyesimama mbele yake ambae pia anatumia mikono kutoa ishara. Mwanamke aliyesimama katikati amevaa hijabu na anaangalia. Upande wa nyuma kuna maduka na msikiti na mwanamke aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau anamsukuma mtoto wa kiume aliyekaa kwenye kitimwendo.]

## Mbinu za msingi zinazohitajika ili kuwa na utetezi wenye ufanisi

> Kuna mbinu tofauti ambazo tunaweza kuzitumia ili tuwe watetezi bora. Baadhi ya mbinu zinazotumika katika tafiti jamii ni muhimu – mbinu hizi ni kama vile kuangalia, kufikiri, na kutenda.

Mchoro uliopo katika ukurasa ufuatao unaonesha jinsi gani tunaweza kutumia mbinu hizi kuwa watetezi bora.


ANGALIA
FIKIRIA
TENDA


[Maelezo ya picha: Mchoro uliopo katika ukusara uliotangulia unaonesha picha tatu tofauti ambazo zimeunganishwa kwa kutumia mshale katika umbo la duara. Picha ya mwanzo kutokea juu inaonesha ngazi ilioandikwa ANGALIA kwa herufi kubwa kuelekea juu ya ngazi na Os zinawakilisha macho. Chini ya ngazi kuna kitimwendo. Picha ya pili kuelekea kulia inaonesha mtumiaji wa kitimwendo na mtu mwengine wote wawili wakiwa na kiduara cha maneno kikionesha kuwa wanawasiliana, na neno TAFAKARI kwa herufi kubwa katika kiwingu cha kufikiria juu ya vichwa vyao. Picha ya tatu inaonesha mtumiaji wa kitimwendo na mwanamke pamoja na mwanamme wakiwa pamoja. Mwanamke amechukua bango linalosema TENDA (CHUKUA HATUA) kwa herufi kubwa.]

[Mchoro uliopo katika ukurasa ufuatao unaonesha picha ndogo ya 'ANGALIA-TAFAKARI-TENDA' katikati na picha tatu kubwa zinazohusiana na kauli hiyo zikiwa zimezunguka picha hiyo. Picha iliyo pembeni ya neno 'ANGALIA' inamuonesha mtu mzima akiwa na mguu mmoja, aliyevaa suti na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama nje ya nyumba . Mlango umefunguliwa. Mwanamke amesimama mlangoni akizungumza na mtu aliye mbele yake. Mwanamke amevaa nguo za kawaida. Anazungumza huku akiashiria na nyusi zake kazipandisha juu – kama mtu anaefafanua jambo fulani. Nyuma yake, kupitia kwenye mlango ulio wazi anaonekana mtoto wa kike aliyevaa kitambaa cha rangi ya pinki kichwani ambae anasafisha sakafu (anapiga deki). Picha inayofuata pembeni ya neno 'TAFAKARI' inaonesha watu watano wakiwa wamekusanyika nje chini ya mti,wanne wamekaa kwenye vigoda na mmoja amesimama. Watu hao ni wanawake watatu na wanaume wawili. Wanawake wawili wamevaa hijabu na mwanamme mmoja amevaa kanzu. Watu hawa watano wanamsikiliza mtu anaezungumza. Mtu huyo amevaa suti, ana mguu mmoja na anatumia gongo la kutembelea. Amesimama. Kando yake kuna filipuchati iliotundikwa kwenye stendi ikiwa na mchoro wa watu wawili – mtoto wa kiume na wa kike wakiwa ndani ya kibanda cha nyasi. Upande mwengine kando ya filipuchati kuna mwanamke aliyesimama akitoa ishara fulani kwa mikono yake. Wote wawili mwanamme na mwanamke wamewaelekea na wanawasiliana na kikundi cha watu watano.


Picha inayofuata pembeni ya neno 'TENDA/CHUKUA HATUA' inaonesha kikundi cha watu watano waliokusanyika pamoja nje. Baadhi yao wamekaa na wengine wamesimama. Mwanamke mmoja amekaa na ameshika fimbo inayotumiwa na wasioona. Mwanamke mwengine aliyesimama anaonesha ishara kwa mikono yake na anawasiliana na mwanamme mtu mzima. Mwanamke aliyevaa nguo za kawaida amesimama kwa nyuma. Watu wote wanamtazama na kumsikiliza

mwanamke aliyevaa kwa umaridadi ambae amesimama, akitabasamu na kuzungumza kwa kutumia kipaza sauti. Mkono wake amemzungushia mtoto wa kike aliyevaa kanzu ya rangi ya zambarau na kandambili huku akiwa amebeba begi. Mtoto wa kike anamuangalia huku akitabasamu. Mwanamme aliyevaa suti mwenye mguu mmoja amekaa kwenye kiti kando ya mwanamke anaezungumza kupitia kipaza sauti. Gongo la kutembelea limewekwa chini. In Nyuma ya picha hii kuna maduka, msikiti, wapita njia na watu waliokaa chini wakionesha bidhaa zao.]




TENDA
FIKIRIA






# 9: Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho katika jamii

**Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho**

- Kupinga mitazamo hasi na imani hasi
- kupeana taarifa na mifano chanya
- Kuwasaidia watu kuelewa kitu fulani tofauti ili ilete maana kwao

## Mitazamo na Imani kuhusu elimu mjumuisho inatokea wapi?




[Maelezo ya picha: picha inaonesha maduara mawili yaliyoingiliana. Katika duara la upande wa kushoto inasema ‘ uzowefu( kilichotutokezea)’ Katika upande wa kulia, inasema ‘maarifa(kile tulichijifunza)’. Katika sehemu ya katikati yalipoungana maduara, inasema ‘ mitazamo & imani (kile tunachofikiri kuhusu vitu tunavyoviamini)’.]

## Baadhi ya mambo muhimu kuhusu mitazamo:

- Ni muhimu kutambua kwamba mitazamo ya mtu mara zote huwa na chanzo.
- Hutegemea mambo ALIYOYAPITIA na ALIYOJIFUNZA (skuli, katika familia, kutoka kwa rafiki zake n.k.)
- Kufahamu aliyoyapitia na kujua alichosomeshwa hutuwezesha kufahamu chimbuko la mtazamo na imani yake kuhusu elimu mjumuisho na kutuwezesha kumuelewa, hata kama hatukubaliani na mtazamo wake.
- Kufahamu kinachobadilisha mitazamo yetu na imani pia hutuwezesha kufahamu kwa nini watu wengine wanadhani au kuamini hivyo wanavyodhani au kuamini.

## Mambo muhimu kuhusu kujenga uelewa:

- Hatuwezi kubadili mitazamo hasi na imani potofu. Bali tunaweza kubadili mitazamo yetu.
- Kufahamu chimbuko la mitazamo yetu kutatuwezesha kupambana na mitazamo hasi na kuimarisha mitazamo chanya kuelekea elimu mjumuisho kwa watu wengine.
- Kwa hivyo kuwa mtetezi wa elimu mjumuisho ni kuwa pia wakala wa mabadiliko ambapo tunajitahidi kupambana na mitazamo hasi na imani potofu na kuimarisha mitazamo chanya.

# 10. Kuendelea kujifunza kuhusu elimu mjumuisho

Mazingira yenye changamoto au magumu yanaweza kuwa fursa kwa ajili ya kujifunza na kubadilika.

Kwa kushirikiana (kufanya kazi pamoja) tunaweza kupata suluhisho kwa urahisi kwenye changamoto tunazokabiliana nazo.



[Maelezo ya picha: wanawake 8 na mwanamme mmoja wakiwa wamesimama kwa mduara. Wako nje. Mwanamke mmoja anaonekana akizungumza huku na waliobaki wanamwangalia na wanamsikiliza.]

- Tafuta fursa katika wilaya yenu ya kukaa pamoja na kujadili changamoto za elimu muumuisho.
- Chunguza katika ngazi ya familia pamoja na wazazi ufahamu wao kuhusu elimu mjumuisho.
- Shirikianeni kutafuta suluhisho la changamoto mnazokabiliana nazo.
- Tembelea skuli za majaribio katika wilaya yako zinazohusika na utekelezaji wa mradi wa elimu mjumuisho.